BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA ARDHI NA MAWASILIANO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika,

Hatuna budi kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana tena katika Mkutano wa Kumi wa Baraza la Tisa kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika,

Nichukuwe nafasi hii pia, kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Mheshimiwa Dkt. Sira Ubwa Mamboya, Naibu Waziri Mheshimiwa Mohammed Ahmada Salum, Katibu Mkuu NduguMustafa Aboud Jumbe, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukitekeleza kazi zetu za kawaida za Kamati.

Mheshimiwa Spika,

Sambamba na hilo, sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati yangu, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya Bajeti ya Wizara hii na hatimae kuyakubali bila ya marekebisho yoyote.

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuheshimu na kuthamini mchango wao mkubwa kwenye Kamati hii hadi kufanikisha kazi hii iliyokusudiwa, naomba niwataje kwa majina Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Suleiman Sarhan Said	-	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Mjumbe
4. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Mjumbe
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Mjumbe
6. Mhe. Mohamedraza Hassanali	-	Mjumbe
7. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Mjumbe
8. Mhe. Said Omar Said	-	Mjumbe
9. Ndg. Fatma Omar Ali	-	Katibu
10. Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir	-	Katibu

Mheshimiwa Spika,

Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imekadiria kukusanya jumla Tshs. 3,749,543,000 bilioni na kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida pamoja na kazi za maendeleo pia imekadiria kutumia Tshs. 214,564,300,000 bilioni. Aidha, fedha hizo zote zitatumika kupitia utekelezaji wa Programu Kuu Tatu (3) na Programu Ndogo Nane (8) zinazokusudiwa kutekelezwa na Wizara hii kupitia taasisi/idara zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika,

Kama alivyoelezaMheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake kwamba matayarisho ya bajeti yake yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (Vision 2020), (Mkuza III), Sera ya Usafiri Zanzibar (2008), Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan), Sera ya Technolojia na Habari (TEHAMA), Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015-2020) pamoja na Maagizo mbali mbali ya Viongozi Wakuu wa Nchi.

Mheshimiwa Spika,

Wizara hii pia imeweka vipaumbele vyake ikiwemo Ujenzi wa Jengo la Kupokelea Abiria (Terminal II), Ujenzi wa Barabara, Ununuzi wa Meli Mpya ya Mafuta, Ununuzi wa Boti Ndogo Ndogo katika Visiwa Vidogo Vidogo pamoja na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano na Huduma zake. Kamati yangu inaunga mkono vipaumbele hivyoilikusaidia kurahisisha huduma za Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya utangulizi huo mfupi niliotoa sasa kwa idhini yako naomba nianza kuingia katika uchanganuzi wa Programu moja baada ya moja ili kuweza kutoa maoni na maagizo ya Kamati juu ya changamoto mbali mbali zilizobainika na kugunduliwa na Kamati wakati wa kupitia Bajeti hii.

PROGRAMU KUU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

Mheshimiwa Spika,
Dhumuni kuu la Programu Kuu hii ni kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri zilizobora, salama na endelevu kwa wananchi wetu wa Zanzibar. Aidha, Programu Kuu hii itatekelezwa chini ya Programu Ndogo (3) ambazo ni Programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji, Programu ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji pamoja na Programu ndogo ya Huduma za Usafirishaji.

Mheshimiwa Spika,
Programu ndogoya Utunzaji na Matengenezo ya Barabarainafanya kazi vizuri, lakini bado inakabiliwa na changamoto kubwa hasa kutokana na ufinyu wa Bajeti kwani ujenzi wa barabara unahitaji fedha nyingi sana wakati bajetitunayoipitisha inakuwa ni ndogo sana na haitoshi kulingana na mahitaji makubwa kwenye majimbo yetu Unguja na Pembapamoja na Ugatuzi kwa baadhi ya barabara na kupelekea barabara hzo za ndani kuwa chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZbado fedha hazitoshi ukilinganisha na mahitaji.

Mheshimiwa Spika,
Mbali ya ufinyu wa bajeti, Idara hii pia, inakabiliwa na uchakavu wa vifaa na mitambo kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara jambo ambalo hupelekea barabara kukosa ubora na uimara hususani wakati wa mvua hali inayosababisha barabara hizo kuharibika na kupelekea barabara kubakia na mashimo makubwa yanayoharibu vyombo vinavyotumia barabara hizo na kuleta usumbufu mkubwa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, uchakavu wa vifaa ni tatizo sugu ambalo hupelekea barabara nyingi kuchelewa kujengwa kwa wakati kutokana na ubovu na kuharibika mara kwa mara kwa vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa barabara. Hata hivyo, Idara hii pia, inakabiliwa na uhaba wa wataalamu na ukosefu wa mafunzo kwa mafundi ambapo haya yote hupelekea kuchelewa kwa ujenzi na matengenezo ya Barabara zetu na pia kupelekea ahadi za viongozi kuchelewa kutekelezwa kwa wakati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika,
Changamoto nyengine ni urasimu uliopo katika upatikanaji wa fedha kutoka Mfuko wa Barabara wakati mwengine hadi kufikia Kamati yako kuingilia kati ili kukwamua hali hiyo. Kutokana na kadhia hiyo, Kamati yangu inaiomba Serikali kuzitafutia ufumbuzi changamoto zote hizo ili programu hii iweze kutekelezwa kwa wakati na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu pi,imegundua kuwa kuna ahadi nyingi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ujenzi wa barabara za majimbo mbali mbali ambazo bado hazijafanyiwa kazi ambapo Mheshimiwa Rais ameshatoa maagizo kwa Wizara husika ikiwemo Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja naOfisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ, hivyo, Kamati yangu tunawaomba muziingize fedha hizo kwenye programu ya ujenzi ili kuhakikisha kwamba ahadi zake hizo zinatekelezwa.

Mheshimiwa Spika,
Pamoja na changamoto hizo tulizozianinisha, Kamati yangu inaitaka Idara kuhakikisha inazikamilisha ahadi zote alizozitoa Mheshimiwa Rais kabla hajamaliza muda wake ili apate kuwaacha vizuri wananchi wake waliompa kura kwa imani kubwa ya kuiongoza Nchi.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu inasikitika kwa kuona kumekuwa na ucheleweshwaji wa makusudi wa Ujenzi wa Barabara ya Wete - Chake ambapo tenda ya Ujenzi huo ilipitishwa tangu mwaka 2009. Awamu ya kwanza ya Ujenzi huoimekamilika miaka karibu 6 iliyopita kwa barabara ya Wete - Konde na Wete - Gando lakini hii ya Wete - Chake imekwama hadi leo. Sambamba na hilo, hadi Kamati hii inapokea taarifa hii kutoka Wizara husika fedha za mfadhili kutoka "Saudi Fund"ziko tayari kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika,
Kukwama kwa utekelezaji huu kunatokana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ndio anayepelekea kuchelewa kwa kushindwa kusaini mkataba ili fedha hizo za ujenzi wa barabara hiyo uweze kuanza. Pamoja na hayo, Kamati yangu itaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulipa fidia wananchi ambao kwa muda mrefu wamezuiwa kutumia au kuyaendeleza maeneo yao ambapo barabara hiyo inatarajiwa kupita.

Mheshimiwa Spika,
Sehemu kubwa ya changamoto nilizozieleza kwenye ripoti ya Kamati ni ufinyu wa bajeti hivyo napenda kuwashauri Wajumbe wenzangu kwakuwa barabara tunazihitaji majimboni mwetu na fedha ni chache, basi ni vyema tukaishauri Serikali kuongeza "Shilingi Mia Moja"ya ziada katika tozo ya Mafuta ili ziingie katika Mfuko wa Barabara ili kuweza kusaidia suala zima lakuongeza ujenzi na ukarabati wa Barabara zetu.

Mheshimiwa Spika,
Aidha, Kamati yangu inaitaka Serikali kuharakisha mchakato wa kuifanya Idara ya Uendelezaji na Utunzaji Barabara (UUB) kuwa Wakala wa Barabara hasa kuzingatia hivi sasa kuna Kampuni nyingi zinazoweza kujenga barabara kwa haraka ili kuondoa changamoto za ubovu wa Barabara zetu.

Mheshimiwa Spika,
Miongoni mwa mambo yanayochangia kuharibika kwa barabara zetu nyingi hasa wakati wa mvua kubwa ni kwamba karibu Barabara zetu zote hazijengewi mitaro ya pembeni ili kupitisha maji ya mvua yaweze kupita pembeni mwa barabara ili kuepusha kutuama kwa maji kwenye barabara matokeo yake hupelekea kuharibika kwa barabara na hatimae kusababisha mashimo makubwa Barabarani wakati wa mvua na pale zinapomalizika.

Mheshimiwa Spika,
Vilevile, kuharibika kwa barabara hizo hutokana na barabara nyingi kushindwa kujengewa pembezoni mwa kingo zake mitaro ya kupitishia maji ambapo barabara nyingi huanza kumong'onyoka, mfano halisi ni ile barabara ya Fuoni iliyojengwa hivi karibuni inaonekana kuanza kumong'onyoka katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika,
Pamoja na Ugatuzi wa Barabara kuipa uwezo Manispaa na Halmashauri kuweza kuingia mikataba na Makampuni binafsi lakini nao wanakabiliwa na ukosefu wa wataalamu katika fani ya barabara kwa hivyo ni vyema ujenzi wowote katika Halmashauri zetu unaokusudiwa kufanyika ni vyema idara hii ya (UUB) ishirikishweili ziweze kusimamiwa na wataalamu wetu na kuepukana kujengewa barabara zisizo kuwa na viwango na pia kuepuka gharama za ujenzi zisizo stahiki.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na Changamoto hizo, Kamati yangu inaomba Serikali pamoja na Wizara husika kuharakisha uandaaji wa Mswada wa Sheria wa Mageuzi ya Idara hii kuwa Mamlaka ili kuipa nguvu zaidi na kuweza kujiendesha wenyewe bila ya kutengemea fedha kutoka Serikalini jambo ambalo litaisaidia zaidi katika kukuza pato la nchi yetu pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika,
Programu ndogo ya pili ya Usimamizi wa Usafiri wa Barabarani, Kamati yangu inaiomba Serikali kuharakisha mchakato wa Karakana ya Magari kuigeuza kuwa Mamlaka ili iweze kuwa na maamuzi na kuweza kuimarisha Karakana hizo kwa vitendea kazi kwa kuipatia mtaji wa kutosha jambo ambalo litaokoa fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Spika,
Kwani hivi sasa magari mengi ya Serikali hupelekwa kwenye "Garage" binafsi kwasababu Karakana yetu haina vifaa vya kutosha, lakini ikigeuzwa kuwa Mamlaka wataweza kuingia katika mikataba itakayowezesha pia usambazaji wa vipuri pamoja kuboresha vifaa vyao na kuboresha mafao ya wafanyakazi wa Karakana hizo za Unguja na Pemba, jambo ambalo litaongeza mapato ya Karakana na kuokoa fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu pia, inaitaka idara kuliweka vizuri eneo la ndani ya karakana kwa kulitia lami hususani katika eneo la kufanyia mtihani wa udereva ili wanafunzi waweze kulitumia vizuri kwani wakati wa mvua hukaa tope nyingi na kupelekea wanafunzi kushindwa kufanya mitihani yao kwa ufanisi kwa ajili ya kupatiwa leseni za udereva na kupelekea Serikali kukosa mapato yatokanayo na upatikanaji wa leseni.

Mheshimiwa Spika,
Sambamba na hilo, Kamati yanguimegundua kuwa maeneo mengi ya Wizara hii kukosa hatimiliki za maeneo husika, maeneo ambayo ndio chachu ya ongezeko la pato la Serikali. Mfano halisi wa hayo, ni idara hii ya Usafiri na Leseni, Shirika la Bandari pamoja na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wa Unguja na Pemba kwani hadi tunaipokea taarifa hii ya bajeti maeneo mengi niliyoyataja hayana hatimiliki jambo linalopelekea wananchi kuanza kuvamia maeneo hayo kwa shughuli zao za kibiashara, kiuchumi na kijamii. Hivyo, tunaiomba tena Serikali kukaa na Taasisi zote hizo pamoja na Kamisheni ya Ardhi juu ya masuala mazima ya upatikanaji wa hatimiliki za maeneo yote niliyoyainisha.

PROGRAMU NDOGO YA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI

Mheshimiwa Spika,
Katika utekelezaji wa Programu Ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji. Kamati pia, inaitaka Wizara pamoja na Mamlaka, Taasisi na Idara husika kufuatilia na kusimamia vyema miradi yote inayokusudiwa kutekelezwa katika mwaka 2018/2019. Miongoni mwa miradi hiyo ni Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara, Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji wa Anga, Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Huduma za Bandari pamoja na Mradi wa Kuratibu Usafirishaji wa Abiria na Mizigo Baharini.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu inasikitishwa sana na tabia iliyojengeka kwa miradi mingi ya Maendeleo ambayo mikataba yake inayopaswa kutiwa saini na Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kucheleshwa kwa makusudi jambo ambalo hupelekea kuchelewa sana utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika,
Kamati imesikitishwa zaidi kuwa hadi inapokea taarifa ya bajeti ya Wizara hii, kuna baadhi ya miradi iliyokusudiwa kutekelezwa katika awamu iliyopita bado imekuwa changamoto na gumzo ndani ya Baraza hili pamoja na wananchi kwa ujumla ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Wete - Chake, Mradi wa Ujenzi wa Terminal II na Mradi wa Bandari ya Mpinga Duri. Ambapo ukiangalia na kwa mwaka huu wa fedha bado miradi hiyo yote imetengewa fedha za utekelezaji ila kwa upande mwengine utekelezaji haonekani jambo linalosababisha Mipango yetu ya Maendeleo kukwama kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu inasikitika sana kwa taarifa tuliyoipata hivi karibuni kuwa" Exim Bank" ya China inayotoa mkopo wa Ujenzi wa Terminal II huenda ikasitisha kutoa fedha za mkopo huu kwa Zanzibar kutokana na ucheleweshaji wa makusudi wa utiaji saini wa mikataba miwili ule wa "Frame Agreement" pamoja na wa "Loan Agreement" uliotengewa fedha za Kimarekani USD.58,347,089 unaotakiwa kusainiwa na Waziri wa Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo mradi huu umeshakubaliwa kila kitu lakini bado kutiwa Saini na Waziri huyo kwa niaba ya Zanzibar na Waziri wa Biashara wa China ambaye anawakilishwa na Balozi wao aliyepo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na mustakbali huo, Kamati yangu huwa inajiuliza masuali mengi yasio na majibu kwani hatujui ni kipi kimekwamisha wakati upande wa mwenzetu miradi hiyo Tanzania Bara inaendelea kwa kasi kubwa jambo hili kwa kweli linasikitisha na kuvunja matumaini kwetu. Hivyo, Kamati inamtaka Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuja kutoa ufafanuzi wa kina juu ya sakata hili kama analijua au laa?Kwani kwa taarifa tulizonazo Kamati kuwa hivi sasa "Technical Committee" na"National Depth Committee" kuwa wameshawasilisha ripoti hiyo kwa Katibu Mkuu zaidi ya miezi miwili hadi leo hajaipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuipitia na kuiwasilisha kwa Waziri wa Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utiaji wa saini.

Mheshimiwa Spika,
Hili ni jambo la kushangaza kwa kuona hivi sasa mjenzi anatumia fedha zake ili mradi usikwame wakati Serikali imeshaahidi kwa miezi 18 kuanzia mwezi Disemba, 2017 hadi Juni, 2019 mradi wa Terminal II ungeliweza kukamilika.

Mheshimiwa Spika,
Kama hatutakuwa makini kuna hatari ya Ujenzi wa Terminal II kama hazikuchukuliwa hatua za haraka ujenzi ukakwama tena kwa mara ya tatu ambapo itakuwa ni aibu kubwa kwa nchi yetu pamoja na Serikali yetu, hivyo, Kamati inamuomba tena Waziri wa Fedha na Mipango kutupatia jibu sahihi ya Suali hili linaloendelea.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, kupitia Programu Ndogo ya Huduma za Usafirishaji Kamati yangu inasikitishwa kuona meli zetu mbili za Abiria zote zimelala mbovu huku wananchi wakikosa huduma za usafiri hasa wa kwenda na kurudi Pemba. Hata hivyo, Kamati yangu inachukua fursa hii kwa kuipongeza Serikali kwa maamuzi ya kuifanyia matengenezo meli ya MV Maendeleo ili kuendelea kutoa huduma kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika,
Pia, Kamati inasikitishwa sana kwa kuona Meli yetu mpya tena ya kisasa kuwa iko nangani imeharibika hadi kutiwa injini nyengine mpya, jambo lililotokana na uzembe mkubwa wa baadhi ya watendaji. Hivyo, tunaitaka Serikali kuunda timu ya Kamati ya wataalamu ili kujua chanzo cha kuharibika kwa meli hiyo na hatua kali za kinidhamu zichukuliwe ili liwe funzo kwa wengine kwa wale wote watakaogundulika juu ya kadhia hiyo. Aidha, Kamati yangu inataka kufahamu jina la Kampuni iliyotengeneza MV.Mapinduzi II na iwapo Kampuni hiyo bado ipo kwasababu inasemekana kuwa Kampuni hiyo imeshafungwa.

Mheshimiwa Spika,
Bado Kamati yangu inaitaka Serikali kutathmini upya suala zima la uendeshaji wa meli hiyo kwani tunahisi inaitia hasara Serikali kutokana na gharama kubwa za uendeshaji wa meli ulinganisha na faida inayopatikana kabla meli hiyo haijachakaa.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yanguinaishauri tena Serikali kuweza kutafuta meli nyengine ya abiria inayoendana na mazingira ya watu wetu na hii iliyopo kuikodisha kwa kampuni za meli za kitalii kwani muundo wa meli tulionayo sasa ni ya kubeba abiria wa kitalii ambao hawabebi mizigo mikubwa, kwanihata ukitazama mfumo wake wa ndani muda wote huhitaji kutumia “Air Conditioner” jambo ambalo ni miongoni wa moja ya changamoto inayopelekea Serikali kutumia fedha nyingi za uendeshaji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika,
Pia, Kamati yangu inalitaka Shirika la Meli kuanzisha “account” maalum ya Mfuko waUendeshaji wa Meli zetu ili muda wowote linapotokezea tatizo na kuhitajika fedha za matengenezo zipatikane kwa wakati. Kwani, Kamati wakati wa kufanya kazi zake imegundua ucheleweshaji wa fedha za vipuri na matengenezo kwa Meli ya MV

Mapinduzi II ndiyo yaliyosababisha meli kushindwa kufanyiwa matengenezo ya haraka, hali inayopelekea meli kulazimishwa kufanya kazi ilihali ni mbovu.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na changamoto hizo, Kamati yangu inashauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kuwashirikisha watendaji wataalamu wa Shirika la Meli kikamilifu katika Mradi wa Ununuzi wa Meli Mpya ya Mafuta tangu katika hatua za awali za manunuzi pamoja na utegenezaji wa meli hiyo pamoja na kuwajengea uwezo wa kitaaluma juu ya uendeshaji wa meli hiyo ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija kwa Taifa.

PROGRAMU KUU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Mheshimiwa Spika,
Programu Kuu hii inatekelezwa kupitia huduma mbali mbali ikiwemo Huduma ya Usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano, Huduma ya Usimamizi wa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano, Huduma ya Usimamizi wa Kituo cha Kuhifadhia Kumbukumbu, Huduma ya Kusimamia Upatikanaji wa Huduma za Tehama Zanzibar pamoja na Huduma ya Uratibu wa Huduma za Mawasiliano ya Simu, "Internet" na Posta Zanzibar ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019 imepangiwa kutumia jumla ya Tshs. 2,893,787,000 bilioni.

Mheshimiwa Spika,
Katika utekelezaji wa programu ndogo pamoja na huduma hizo nilizoziainisha katika programu hii kuu Kamati yangu inaishauri Idara ya Mawasiliano pamoja na Wizarahusika vile vituo vyote vya Tehama jamii vilivyojengwa kupitia mradi wa huo (UCSAF) kwa upande wa Unguja na Pemba kuvikabidhisha kwa Wakuu wa Wilaya husika kwa ajili ya kuvisimamia, kuvienzi na kuviendeleza kwa kushirikiana na Halmashauri za kila Mkoa, hasa kwa kuzingatia Idara hii hapo baadae hawatokuwa na bajeti ya kuviendeleza vituo hivyo kwa hiyo kuvikabidhi Halmashauri wataweza kuvisimamia na kuviendesha vyema.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, Kamati yangu inaiomba tena Idara kwa kushirikiana na Wafadhili wa Mradi huu wa vituo vya Tehama jamii katika awamu ya pili ya utekelezaji kuviangalia kwa jicho la karibu kwani bado vituo hivyo vyote vilivyojengwa kwa ajili ya kuisaidia jamii kwa upande wa Unguja na Pemba vinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vyoo kwani kukosekana kwa vyoo kutapeleka uharibifu wa mazingira pamoja na maradhi ya mripuko katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu pia, inaitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa upande wa Zanzibar kushirikiana na Idara ya Mipango, Sera na Tafiti ya Wizaraili kuhakikisha kabla ya kupitisha Mkonga kufanya tathmini ya kina ili kuepuka kukatwa mara kwa mara hasa kunapotokea ukarabati au ujenzi wa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, Kamati yangu imefurahishwa sana na maamuzi ya kuurejesha Mkonga wa Mawasiliano kwa Serikali kwani kwa kipindi chote ulipokuwa umekabidhiwa Kampuni ya Zantel, Serikali haikupata faida yoyote inayotokana na mapato. Hivyo, tunaamini kwamba kurejeshwa kwa Mkonga huo, Serikalini sasa tutaweza kupata tija kubwa pamoja na hayo Kamati yangu inataka ufanywe utafiti wa kina ikiwa Zantel walitumia Mkonga huo kwa kukusanya mapato na kuikosesha Serikali mapato hayo basi ni vyema wakaipatia Serikali kiwango ambacho walikusanya kwa niaba yetu.

Mheshimiwa Spika,
Sambamba na hayo, Kamati yangu pia, imegundua kuwa mfumo uliotumika kuunga Mkonga wetu wa Mawasiliano ulikuwa unamakosa ya kitaalamu kwani ikiwa mteja aliyeungiwa mwanzo umeme ukikatika basi na yule mteja anayefuata na yeye anakosa mawasiliano kutokana na kasor0, hivyo, ni vyema Serikali iandae utaratibu maalum wa kuzirekebisha kwa matumizi bora na endelevu kwa nguvu kazi ya Taifa hili.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI

Mheshimiwa Spika,
Katika mwaka wa fedha 2018/2019 programu ndogo hii imepangiwa kutumia Tshs. 1,687,083,000 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa huduma muhimu za Wizara ikiwemo Huduma ya Ununuzi wa Vifaa vya Ofisi na Huduma ya Usimamizi wa Rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika,
Kupitia programu ndogo hii, Kamati yangu inaendelea kuishauri Serikali na Wizara husika kuhakikisha katika fedha hizo ununuzi wa mtambo wa kuchanganyia lami unakamilika ili kuweza kuutumia kwani uliopo hivi sasaunashindwa kufanya kazi ipasavyo ambapo mara kwa mara unaharibika ambapo mara kwa mara kazi hukwama na kupelekea Idara kukodi mtambo wa mtu binafsiilikumalizia kazi iliyopo jambo linalopelekea kutumia fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, kwa kuwa Kamati yangu imebaini kuwa maeneo mengi yaliyo kwenye taasisi zilizomo katika Wizara hii hazina hatimiliki kwa hiyo ni vyema Wizara ikakaa na taasisi zilizomo katika Wizara hii ili kuandaa utaratibu maalum wa ufuatiliaji wa upatikanaji wa hatimiliki hizo kwa manufaa ya nchi kwa jumla.

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA

Mheshimiwa Spika,
Idara hii ndio kiungo maalum katika Wizara kwani kama inavyofahamika kuwa mipango yote ya Wizara inabidi iratibiwe na idara hii halafu kutolewa mikakati ya utekelezaji kwa kila taasisi husika.Pamoja na hayo, Kamati pia, inaiomba Idara hii muhimu ya Mipango, Sera na Tafiti inapofikia wakati wa utekelezaji wa miradi inayohusu sehemu husika kuweza kuwashirikisha wataalamu na watendaji wa sehemu hizo ili yasijejitokeza kama yaliyojitokeza katika Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Terminal II na Ununuzi wa Meli ya MV. Mapinduzi II kwani kutowashirikisha kikamilifu hatimae ni kuiingiza Serikali yetu katika hasara.

Mheshimiwa Spika,
Pia, Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara zake zote kuwatumia ipasavyo Wakala wa Majengo wa Serikali na Bodi zake katika miradi yetu yote kabla ya kuanza utekelezaji kwani wao ndio wasimamizi wakuu kwa mujibu wa Sheria katika majengo yote ya Serikali na hatimae kuweza kuishauri Serikali kitaalamu.

Mheshimiwa Spika,
Kutofanya hivyo ni kuitia hasara kubwa Serikali kwa kujengewa majego yasiyokuwa na kiwango, ubora na uimara wowote hali inayopelekea kuhatarisha maisha ya wananchi wetu pamoja na viongozi wetu kiujumla.

Mheshimiwa Spika,
Mwisho kabisa,Kamati ya Ardhi na Mawasiliano imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019, na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako wote waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika,
Napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena viongozi na watendaji wa Wizara hii tena kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao

kwa Kamati hii. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika,
Baada ya maelezo hayo naiunga mkono bajeti hii na naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……,
Hamza Hassan Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ardhi na Mawasiliano,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar